



23 Agosti, 2021

**MARUDIO**  
**TANGAZO LA ZABUNI YA UKUSANYAJI WA USHURU MWAKA WA**  
**FEDHA 2021/2022**

Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe inakusudia kuweka wakala wa ukusanyaji wa ushuru katika vyanzo mbalimbali vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Korogwe anapenda kuwatangazia watu binafsi, Makampuni, Mashirika au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

NAMBA YA ZABUNI	LOT	ENEO LA UKUSANYAJI
KDC/LGA/125/2021/2022/NCS/LOT 01-06	LOT 01	Kukusanya ushuru wa mazao ya Chakula
	LOT 02	Kukusanya ushuru wa mazao ya biashara-isipokuwa chai na Mkonge
	LOT 03	Kukusanya ushuru wa stendi/Maegesho-Mombo
	LOT 04	Kukusanya ushuru wa mazao ya Misitu
	LOT 05	Kukusanya ushuru wa madini ya Ujenzi(kokoto,mchanga,Mawe na Kifusi n.k)
	LOT 06	Ukusanyaji wa Ushuru wa Machinjio

Zabuni hizi zipo wazi kwa Mwananchi na Wakazi wote ambao ni Raia wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, na zitaendeshwa kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma(bidhaa,ujenzi,huduma zisizo za kiushauri na utekelezaji wa mali chakavu za Umma kwa zabuni) Sheria na.7 ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2013 G.no.446 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016.

## MASHARITI YA ZABUNI

1. Maombi ya Zabuni ni Tsh.50,000/= zitalipwa kwenye akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe baada ya kupewa Control Number na hazitarejeshwa.
2. Muombaji awe leseni ya biashara husika, leseni inayohusu biashara ya kazi uliyoomba katika eneo utayoombea kazi.
3. Muombaji awe na uwezo wa kifedha/Mtaji wa biashara, kwa ajiri ya kugharamia kazi nzimz ya ukusanyaji(weka benk statement ya miezi mitatu ya karibuni).
4. Muombaji awe ambatanishe nyaraka za kisheria (Power of Attorney)kwa kazi anayomba.
5. Muombaji aonyeshe mahali ofisi yake ilipo (Physical Address)ili kuwa rahisi kujua uhalali wa kampuni yake na kuweza kupatikana kwa ulahisi.
6. Makusanyo yote yatawasilishwa Halmashauri kabla ya kulipwa kamisheni kutoka kwenye makusanyo aliyowasilisha.
7. Tathimini itazingatia vigezo vyote vilivyopo vya zabuni pamoja na bei kulingana na bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
8. Watakao shinda zabuni hii wanapaswa kuleta dhamana ya utendaji kazi (performance bond) kabla ya kuanza kufanya kazi hiyo.
9. Maombi yote yajazwe kwa umakini na nyaraka (company profile) na ifungwe vizuri kwenye lakiri ndani ya bahasha.
10. Muombaji ataje kiwango ambacho ataikusanyia Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ambacho kitakuwa ni kigezo moja wapo cha muombaji kupata kazi.
11. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 09/09/2021 saa 4.00 Asubuhi, Ofisi ya **Mkurugenzi Mtendaji** iliyopo Kwasunga, katika Kitengo cha Manunuzi na Ugavi.

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
S.L.P 584  
KOROGWE.**

*Habiba S. Mtunguja*  
**Habiba S. Mtunguja**  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

2

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**S.L.P 584**  
**KOROGWE**